BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Tano – Tarehe 18 Februari, 2025.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

95. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

    Tathmini iko vipi juu ya viwango vya juu vya ongezeko la joto na athari zake kwa kipindi cha miezi 3 iliyopita.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

147. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kazi kubwa na nzuri ya kuimarisha miundombinu ya barabara kwa kujenga barabara mpya na za kisasa. Hata hivyo katika kuufanya mji upendeze zaidi pamoja na barabara hizo, upandaji wa miti kando ya barabara ni muhimu.

Je, ni lini hasa wazo la kupanda miti kandokando ya miundombinu mipya ya barabara zetu litaanza rasmi ili kuuweka mji wetu kwenye haiba na hadhi yake.

## Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

79. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini ni jambo la lazima kwa taasisi za Serikali na hata taasisi binafsi.

Je, kwa kiwango kipi Serikali imefanya ukaguzi na kujiridhisha kuwa jambo hilo linafanyika kikamilifu kwa taasisi hizo.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

32. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kuamini katika msimu mkubwa na msimu mdogo kwenye ushindani wa sekta ya utalii ni jambo ambalo linaweza kutupunguzia mapato ya fedha za kigeni.

Wizara inachukua jitihada gani ili kupambana na mawazo hasi ya kuamini uwepo wa msimu mdogo katika kuukuza utalii wetu.

89. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa kuna wimbi kubwa la wafanyakazi wa kigeni kufanya kazi za mahoteli, mawakala wa utalii na watembeza wageni na kulipwa mishahara mikubwa ya fedha za kigeni. Na kwa kuwa nafasi zinazotolewa kwa wageni hao zinaweza kujazwa na wazawa na hivyo kuendelea kuwakosesha wazawa hao ajira na kuitumikia nchi yao.

Je, Wizara yako kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji inafanya nini kutatua tatizo hili, huku ikizingatiwa kuwa ni suala la muda mrefu lisilotatuliwa kikamilifu.

<u>**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**</u>

155. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni aina gani za mazao kwa sasa yamefanyiwa utafiti wa kuwa na uwezo wa kuhimili wadudu, magonjwa na ukame ili kuweza kuongeza tija

<u>**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**</u>

73. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika shehia ya Michamvi Kae, umekuwa ni tatizo kwa wananchi wa eneo hilo.

(a) Je, Serikali inalifahamu vipi tatizo hilo.

(b) Je, kuna mikataba yoyote ya ufumbuzi wa tatizo hilo.

(c) Je, ni lini utakwenda kukutana na wananchi hao ili waweze kufahamu jinsi Serikali inavyochukua jitihada za ufumbuzi wa suala hilo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

58. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Uhaba mkubwa wa vyuo vya taaluma ya michezo na upungufu wa wataalamu wa michezo unaweza kuzorotesha malengo ya baadae ya maendeleo ya sekta ya michezo.

    Ni yepi na upi mtazamo wa Wizara katika kuona kwamba inaendelea kupambana na changamoto hii.

59. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya kazi kubwa ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo katika muonekano bora na wakisasa.

    Je, Wizara imejipanga vipi katika usimamizi na utunzaji wa viwanja hivyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

123. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Ujenzi wa skuli za ghorofa ni kielelezo tosha cha mageuzi makubwa katika sekta ya elimu Zanzibar.

    Kwa kiasi gani suala la utunzaji na uendelezaji wa majengo haya unazingatiwa.

137. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Tathmini ya uwiano wa walimu kwa wanafunzi iko vipi na ina mchango gani katika kuongezeka kwa viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka 2024.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

2. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wakati wa ujenzi wa barabara ya Wete ya kilomita 22.1 walikuwepo wananchi wakiwemo wa jimbo la Mtambwe ambao waliingia katika kundi la kupatiwa fidia ya nyumba na wengine fidia ya miti. Pamoja na juhudi za Serikali kulipa fidia ya nyumba, bado wananchi hawajapata fidia ya miti iliyong'olewa wakati wa ujenzi wa barabara.

(a) Ni wananchi wangapi ambao bado hawajapata fidia hii kulingana na tathmini ya Serikali.

(b) Ni lini Serikali itawalipa wananchi ambao wanastahili kulipwa fidia hii.

124. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

(a) Ni lini mradi mkubwa wa kimkakati wa 'taxes' za baharini Zanzibar unatarajiwa kuanza.

(b) Kwa kiasi gani mradi huu utaongeza zaidi thamani ya ukuaji wa soko la utalii nchini.

(c) Ni kwa vipi mradi huu utarahisisha na kufungua mawasiliano ya ndani hususani katika mzunguuko wa visiwa vidogo vidogo.

**Wizara ya Afya:**

67. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali imeweka '*lift*' ndani ya hospitali zetu kwa lengo la kuwarahisisishia wananchi wetu kupanda na kushuka wakati wa kuwaangalia wagonjwa wao. Katika hospitali yetu ya Lumumba kumebainika changamoto ya walinzi kuwazuia wananchi wanaotaka kuzitumia '*lift*' hizo wakati wa kushuka chini mara tu wanapomaliza kuangalia wagonjwa wao.

(a) Je, kwa kiwango kipi Serikali inaitambua changamoto hii.

(b) Ni zipi sababu za msingi zinazopelekea walinzi katika hospitali hii ya Lumumba kuwazuia wananchi kuzitumia '*lift*' hizi wakati wa kushuka mara tu wanapomaliza kuwangalia wagonjwa wao.

121. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je kuna ukweli gani juu ya matumizi ya vyombo vya plastiki kuwa na madhara ya kiafya kwa binadamu pindi akivitumia.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

51. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Fursa za Uchumi wa Buluu zilizopo nchini bado hazijatumika ipasavyo kutokana na changamoto mtambuka ambazo ni vigumu kutatuliwa na sekta moja.

Je, ni upi mtazamo na mkakati wa Serikali juu ya mtazamo kama huo.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**18 Februari, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**